

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخَلَفَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يُكِنْهُمْ هُنَّ دِينُمُ الَّذِي أَرْضَى لَهُمْ وَلَمْ يُبَدِّلُنَّهُمْ فَإِنَّمَا يَعْذِذُونَ
لَا يَشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ



Jumapili, 22 Jumada I 1446 H

24/11/2024 M

Na: HTS 1446 / 26

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Waziri wa Masuala ya Kidini na Wakfu awa Mgeni wa Hizb ut Tahrir

(Imetafsiriwa)

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir/Wilayah Sudan ukiongozwa na Ustadh Nasser Ridha (Abu Ridha), Mkuu wa Kamati Kuu ya Mawasiliano ya Hizb ut Tahrir katika Wilaya ya Sudan, na pamoja naye Ustadh Ibrahim Othman (Abu Khalil), Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir katika Wilayah ya Sudan, na msaidizi wake, Ustadh Muhammad Jameh (Abu Ayman) ulimpokea Ndugu Dkt. Omar Bakhit Muhammad Adam, Waziri wa Masuala ya Kidini na Wakfu wa Kifederali katika afisi ya Hizb mjini Port Sudan, jana, Jumamosi, 21 Jumada al-Awwal 1446 H sawia na 23/11/2024 M.

Mwanzoni mwa hotuba yake, Ustadh Nasser alimkaribisha Waziri, akawatambulisha wajumbe, kisha akazungumza kwa kuitambulisha Hizb ut Tahrir, ambacho ni chama cha kisiasa, kinachotaka kuanzisha tena maisha kamili ya Kiislamu kuititia kusimamisha Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, akitilia mkazo faradhi ya kuifanya kazi Khilafah, na kwamba hizb inafuata njia ya Mtume, (saw), katika kusimamisha dola; kuanzia kusimamisha chama chenye msingi wa Uislamu, kisha kuingiliana na jamii kuititia mivutano ya kifikra na mapambano ya kisiasa, kisha kutafuta nusra kutoka kwa watu wenye nguvu na uwezo.

Kisha Ndugu Nasser akazungumza juu ya kile ambacho Magharibi, haswa Marekani, inapanga kuifanya misikiti na jumuiya za Kidini zifanye kazi kwa mujibu wa matamanio yake, na anachokusudia kafiri ni kubadili mazungumzo ya kidini.

Kisha yule ndugu waziri akazungumza, akithamini dori ya Hizb ut Tahrir, lakini anaona kwamba wakati unahitaji kusimama pamoja Jeshi. Ndugu Nasser alieleza ruwaza ya kisheria na kisiasa ya vita hivi.

Mwishoni mwa mkutano huo, ilisisitizwa kuendelea kwa mikutano hii.

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Sudan**